TANGAZO LA SERIKALI NA. 325 la tarehe 26/4/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MATANO KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI KWA KAMPUNI YA EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE LIMITED YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Matano kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kwa Kampuni ya East African Crude Oil Pipeline Limited ya mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika kuanzia tarehe 6 Machi, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa Magari Matano yaliyoanishwa katika Jedwali la Amri hii, zilizoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na Kampuni ya East African Crude Oil Pipeline Limited kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa Magari hayo yatatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yaliyotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 5 Septemba 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Aina | Chassis Na. | Injini Na. |
|---|---|---|---|
| 1. | Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4 | 6FPRXXMAWRPU70891 | YNWQRPU70891 |
| 2. | Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4 | 6FPRXXMAWRPU70892 | YNWQRPU70892 |
| 3. | Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4 | 6FPRXXMAWRPU70893 | YNWQRPU70893 |
| 4. | Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4 | 6FPRXXMAWRPU70894 | YNWQRPU70894 |
| 5. | Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4 | 6FPRXXMAWRPU72988 | YNWQRPU72988 |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

Dodom
4 Aprili, 2024.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*